



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. BA.170/318/01/43

27 Aprili 2026

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA (RADIOLOJIA) – NAFASI 02

Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kupitia Divisheni ya Afya, Ustawi wa jamii na Lishe na kwa kuzingatia mwongozo wa Kitaifa wa kujitolea kwa wataalamu wa Afya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kuomba nafasi ya mkataba kwa taaluma ya MTEKNOLOJIA WA MIONZI DARAJA II – RADIOGRAFA (RADIOLOJIA).

SIFA ZA MWOMBAJI NA MASHARITI YA JUMLA

- I. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri wa miaka 18 mpaka 45
- II. Mwombaji aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
- III. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees, wataalamu kuaminika pamoja na namba za simu)
- IV. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, na vilivyothibitishwa na wakili au Kamishna wa viapo
- V. Testimonies, provision result, statement of results havitakubaliwa
- VI. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanywa ulinganishi na TCU na NACTE
- VII. Kwa waombaji wote wa nafasi ya **Mteknolojia II** mnaelezwa kuambatisha leseni iliyohuishwa
- VIII. Waombaji waambatanishe picha moja passport size ya hivi karibuni
- IX. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza.

Uk. 1

Mtaa wa Kakora, S.L.P 88, Ngudu, SIMU : +255 (028) 2983121, Nukushi: +255 (028) 2983119
Barua Pepe: ded@kwimba dc.go.tz , dhro@kwimbadc.go.tz , Tovuti: www.kwimbadc.go.tz

- X. MUHIMU:Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti. Aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe na kutumwa kwa njia ya Posta au yawasilishwe Ofisi ya Masijala ya Wazi kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 88,
NGUDU – KWIMBA.

- XI. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

MAJUKUMU NA KAZI ZA MTEKNOLOJIA DARAJA II – RADIOGRAFA (RADIOLOJIA)

- I. Kuwapima wagonjwa wanaoelekezwa kwenye eneo lake la kazi
- II. Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi
- III. Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (diagnostic quality)
- IV. Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa
- V. Kusimamia watumishi walio chini yake
- VI. Kutoa ushauri kuhusu masuala ya kazi na Radiolojia na mionzi katika eneo lake la kazi (sterilization)
- VII. Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi
- VIII. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

NGAZI YA MSHAHARA TGHS B1

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali katika ngazi ya TGHS B1 kwa mwezi na kama ilivyoelekezwa katika mwongozo wa Kitaifa wa kujitolea kwa wataalamu wa Afya kwa waombaji wa nafasi za Mkataba watalipwa nusu mshahara ya nafasi husika iliyotangazwa.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 31 Mei 2025.

Imetolewa na



Dkt. Amon Mkoga

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

Mtaa wa Kakora, S.L.P 88, Ngudu, SIMU : +255 (028) 2983121, Nukushi: +255 (028) 2983119
Barua Pepe: ded@kwimba.dc.go.tz ,dhro@kwimbadc.go.tz , Tovuti: www.kwimbadc.go.tz

Uk. 2